# 24. KUZALIWA KWA YOHANA MBATIZAJI

*“Na wengi katika Waisraeli atawarejeza kwa BWANA Mungu wao”*

## Shabaha

Kuonyesha jinsi Zakaria na Elisabeti walivyopata mwana katika uzee wao ambaye ni mtangulizi wa Masihi. Kama tulivyoona, Hagai na Zakaria walikuwa manabii waliorudi kutoka Babeli katika mwisho wa miaka sabini ya utumwa.Waliwatia moyo watu kujenga tena nyumba ya Mungu na wakairudisha ibada ya kweli ya kumwabudu BWANA. Na nabii wa mwisho katika Agano la Kale alikuwa ni Malaki. Alitabiri wakati wa Nehemia, ambapo tatizo lililokuwa kubwa katika Yuda ilikuwa ni kuoa mtu ambaye yuko nje ya Kweli. Kuoana na mtu aliye nje ya Kweli ni moja ya njia rahisi sana ya kuwageuza watu wa Mungu na kuwapeleka kwenye ibada ya uongo, na Malaki aliwaonya kwa nguvu sana kuhusu jambo hili. Alikuwa ni nabii wa mwisho ambaye Mungu alizungumza na watu wake kupitia yeye kabla ya kuja kwa Yohana Mbatizaji. Kwa karibu miaka mia sita Israeli walitawaliwa na mataifa nyenye nguvu: Babeli, Uyunani, Uajemi na hatimaye Rumi, kama vile Mungu alivyokuwa amemwonyesha Nebukadreza katika ndoto yake. Wayahudi walitamani sana waweze kuwa huru wasitawaliwe na mataifa mengine. Lakini kama wangetambua, kwamba Mungu ndiye aliyekuwa ameyaleta mataifa haya kuwaadhibu Israeli ili kuwanyenyekeza wamgeukie Mungu. Na kama kawaida, walikuwapo watu wachache waaminifu katika Israeli ambao waliendelea kusoma torati na manabii. Watu hawa wanaume na wanawae walisubiri kwa hamu sana kuja kwa Masihi, “**Mpakwa mafuta”** wa Mungu. Waliamini kuwa atakuja Masihi ambaye angewaweka huru. Wao walizitama ishara katika mambo ya ulimwengu, kama tunavyofanya leo, kwa maana tunaamini kwamba Kristo, “**Mpakwa mafuta”** mfalme wa Israeli, atakuja upesi mara ya pili.

Luka 1:5-25,57-80

## ZAKARIA NA ELISABETI: Luka 1:5-7

Miongoni mwa watu waliokuwa wanangojea kwa ajili ya kuja kwa Masihi alikuwa ni kuhani mwaminifu wa Mungu, aliyeitwa jina lake Zakaria. Yeye na mke wake Elisabeti walimtumikia Mungu kwa furaha. **“Na wote wawili walikuwa wenye haki mbele za Mungu, wakiendelea katika amri zote za BWANA na maagizo yake bila lawama”** (mstari 6). Jambo moja lililowavunja moyo wakati wote-hawakuwa wamebarikiwa kupata watoto. Na sasa, wote wawili wakawa wamezeeka naye Elisabeti alikuwa amekwishapita umri wa kuweza kuzaa. Siyo tu kwamba walimwomba Mungu awapatie watoto, bali pia walimwomba aje Masihi. Hili lilikuwa ombi lao la kila wakati.

## ZAKARIA AKIWA KATIKA HEKALU: Luka 1:8-22

Miaka mingi iliyokuwa imepita, Daudi alipanga utaratibu wa huduma katika nyumba ya Mungu, aliwapanga makuhani katika zamu ishirini na nne, ili kila kuhani awe na zamu aingie kufanya kazi ya ukuhani katika katika nyumba ya Mungu (1Mambo ya Nyakati 24:19).

Wakati zamu ya Zakaria ilipofika, huduma yake ilikuwa ni kufukiza ubani katika Patakatifu. Nje, watu walikuwa wakisali wakati wa kufukiza uvumba.

Ghafla, Zakaria alipokaribia madhabahu ya kufukizia uvumba, malaika wa Mungu akamtokea, alikuwa amesimama upande wa kulia wa madhabahu ya kufukizia uvumba. Kuonekana kwa malaika yule kulimwogopesha sana Zakaria, lakini malaika akamwambia: **“Usiogope, Zakaria, maana dua yako imesikiwa, na mkeo Elisabeti mtoto mwanamume, na jina lake utamwita Yohana”** (mstari 13). Siyo Zakari na Elisabeti peke yao watakaofurahia tu, bali malaika alisema wengi watafurahia kuzaliwa kwa huyo mtoto. Angekuwa ni mtoto maalumu, maana Mungu alikuwa na kazi kubwa ambayo angeifanya. Na kwa sababu ya kazi yake maalumu,hataruhusiwa kunywa divai wala mvinyo. (Utakumbuka kwamba jambo kama hili la kukatazwa na Mungu lilitokea katika suala la Samsoni –Waamuzi 13:4-5 na Hesabu 6:2-3) mawazo ya Yohana yalitakiwa kila wakati yawe yamwelekee Mungu, ili afikirie tu kufanya kazi aliyopewa na Mungu. Kazi hii ilikuwa ya mhimu na hivyo; **“naye atajazwa Roho Mtakatifu”** hata tangu hajazaliwa (mstari 15). Kazi hii maalumu ili ni ipi

ambayo angeifanya kwa ajilo ya Mungu iliyohitaji maandalizi makini kuanzia wakati wa kuzaliwa kwake?

Malaika alimwambia Zakaria kuwa mtoto huyu, ambaye yeye na Elisabeti watamzaa katik uzee wao, alikuwa ndiye ambaye **“atamwekea Bwana tayari watu waliotengenezwa”** (mstari 17). Maana yeye alipaswa kumtangulia Bwana Yesu Kristo. Alipaswa awe mtangazaji, ambaye angewatangazia habari njema kwa wana wa Israeli kwamba anakuja Masihi. Mioyo ya watu ilitakuwa kutayarishwa ili wampokee. Walikuwa wameishi miaka mia nne bila ya kuwa na nabii wa Mungu katikati yao. Kwa hiyo ilimpasa mtu mmoja kuyaandaa mawazo ya watu wampokee Masihi. **“Na wengi katika Waisraeli atawarejeza kwa BWANA Mungu wao”** (mstari 16)

Zakaria alifadhaika sana. Hakuamini hata aliyoyasikia, **“Nitajuaje neno hilo?”** alimwuliza mjumbe wa Mungu aliyekuwa amesimama mbele yake, **“maana mimi ni mkongwe wa siku nyingi”** (mstari 18). Malaika alimjibu kwa kujitabulisha alikuwa ni nani. Mimi ni Gabrieli nisimamaye mbele za Mungu (mstari 19). Huyu alikuwa ni malaika aliyewahi kumtokea Danieli katika Babeli mamia ya miaka iliyopita (Danieli 8:16, 9:21). Huyu malaika alimfahamisha Danieli kuhusu kuja kwa Masihi na sasa alikuwa anamfahamisha Zakaria kwamba mwana wake ndiye atakayetangaza kuwa Masihi amekuja / Bila shaka Zakaria alishangazwa na ujumbe huu. Malaika aliendelea kumwambia Zakaria ishara atakayo kuwa nayo.

**“Na tazama, / utakuwa bubu, usiweze kusema, mpaka siku ile yatakapotokea hayo, kwa sababu hukayasadiki maneno yangu; nayo yatatimizwa kwa wakati wake”** (mstari 20). Hii ilikuwa ndiyo iwe ishara kwa Zakaria na kwa wote waliomfahamu, ya kwamba hakika huo ulikuwa ni ujumbe uliotoka kwa Mungu.

Na nje watu walikuwa wanasubiri, walishangaa kwa nini Zakaria alichelewa sana. Na hatimaye alipotoka, alikuwa hawezi kuwaambia yaliyompata, maana kama malaika alivyosema, alikuwa bubu, hata hivyo ilikuwa ni wazi, kwa jinsi alivyoonekana na akionyesha ishara kuwa ameona maono ndani ya nyumba ya Mungu.

## ELISABETI ANAPATA MWANA: Luka 1:23-25,57-66

Wakati zamu yake ya huduma katika yumba ya Mungu, alirejea nyumbani kwake katika nchi ya vilima y Yudea. Yeye na mke wake Elisabeti walisubiri kwa hamu sana kuzaliwa kwa mwa mwao huko. Mwisho, muda wa furaha ukafika, na rafiki zake wote na jamaa zake walikusanyika pamoja kushiriki furaha yao. Walifurahia kusikia kwamba Bwana **“amemwongezea rehema zake”** (mstari 58), kwa kumpatia Elisabeti mwana katika uzee wake.

Na kama ilivyokuwa desturi katika Israeli, mtoto huyu mchanga wa kiume alitahiriwa siku ya nane, na kila mmoja alifika wakafurahi pamoja. Wote walitarajia kuwa mtoto ataitwa Zakaria, jina la baba yake. Hata hivyo Elisabeti, alikuwa ameshamwelewa Zakaria ya kwamba malaika Gabrieli alikuwa tayari amesha mpa jina Yohana. Elisabeti akasema, **“ataitwa Yohana”** maana yake **“neema ya Mungu”.** Kila mmoja akastaajabu, maana katika jamaa zao hakuwapo mtu aliyeitwa jina hilo. Ndipo wakamwashiria Zakaria, ili wajue yeye alitaka amwiteje. Kwa kuwa bado hakuweza kusema, walimpatia ubao ili aandike na aliandika vizuri: **“Jina lake ni Yohana”** (mstari 63). Kila mmoja alishangaa; na wakashuhudia jambo la kuwahofisha zaidi. Ghafla Zakaria akaweza kusema tena / Baada ya miezi tisa ya ukimya, **“ulimi wake ulifunguliwa, akaanza kunena na kumsifu Mungu”** (mstari 64). Hakika huu ulikuwa ni mwujiza na waliogopa sana, kwa kuwa hili lilikuwa ni jambo ambalo hawakulielewa. Habari ya tukio hili ikatangazwa katika wilaya zote haraka na kila mmoja akastaajabu, **“Mtoto huyu atakuwa ni wa namna gani?”** (mstari 66)

## ZAKARIA ANATABIRI: Luka 1:67-80

Zakaria hakuweza kusema tena tu, bali pia alijazwa na Roho Mtakatifu, na akatabiri. **“Atukuzwe Bwana, Mungu wa Israeli”** (mstari 68). Alisema kuhusu Masihi, ambaye ni Yesu tunayemjua, ambaye alikuwa hajazaliwa wakati huo. Mungu alikuwa ameshatabiri miaka mingi iliyokuwa imepita kwamba atawatumia Israeli mwokozi, kama alivyokuwa amemwahidi Ibrahimu na Daudi (Mwanzo 22:17-18; 2 Samweli 7:12-16). Na sasa alikuwa amekaribia kulitimiza Neno lake na Yohana alikuwa ndiye atangulie mbele yake akiwa na habari hii

njema. **“Nawe, mtoto, utaitwa nabii wake Aliye juu, Kwa maana utatangulia mbele za uso wa Bwana umtengenezee njia zake”** (mstari 76)

Kuanza kwa matukio haya ulikuwa ndiyo mwanzo maajabu mengi katika Israeli. Mtoto alikua na **“mkono wa Bwana ulikuwa pamoja naye”** (mstari 66).

Kisha akakaa majangwani akangojea huko mpaka alipokuwa tayari kuwatokea na kuwatangazia Waisraeli wote.

## FUNDISHO KWETU

Zakaria na Elisabeti ni mfano wa mzuri sana kwetu. Katika mwenendo wao walikuwa ni wanyenyekevu, wakizitii amri zote za Mungu. Waliomba kila wakati, siyo tu kwa yale waliyokuwa wanayataka, bali waliomba hata kwa ajili kutimizwa kwa kusudi la Mungu hapa duniani. Walifahamu kuwa kuja kwa Mwana wa Mungu aliyeahidiwa italeta faraja kubwa na furaha kwa wote wawili na kwa Israeli wote, lakini hawakuhi kuota ndoto kamwe kwamba wao wenyewe watahusika katika kutokea kwake. Walikuwa ni watu wanyenyekevu na ni watu wa aina hiyo ambao Mungu anawachagua.

Hata sisi tunapaswa kuzionyesha sifa za aina hii katikamaisha yetu, ili kwamba Bwana Yesu Kristo atakapokuja mara ya pili, tusiwe na hofu wakati mjumbe wake atakapotuita kukutana naye.

## MAELEZO YA ZIADA

Kuja kwa Yohana Mbatizaji kulikuwa kumeshatazwa na manabii miaka mingi kabla ya kuzaliwa kwake. Zakaria alikuwa akijua vizuri kabisa maneno ya Isaya: **“Sauti ya mtu aliaye nyikani, itengenezeni njia ya Bwana”** (Isaya 40:3)

Malaki pia alinena habari zake: **“Angalieni, namtuma mjumbe wangu, naye ataitengeneza njia mbele yangu; naye Bwana mnayemtafuta atalijilia hekalu lake ghafla; naam, yule mjumbe wa agano mnayemfurahia, angalieni, anakuja, asema BWANA wa majeshi”** (Malaki 3:1)

## MASWALI

### Majibu Mafupi

1. Zakaria na Elisabeti walikuwa ni watu wa namna gani?
2. Zakaria likuwa akifanya nini katika nyumba ya Mungu?
3. Watu walikuwa wanafanya nini nje ya hekalu?
4. Ni nani aliyemtokea Zakaria katika nyumba ya Mungu?
5. Ni jambo gani ambalo malaika alisema kwamba lingemfanya Zakaria na Elisabeti?
6. Ni kazi ipi kubwa ambayo Mungu alikusudia ifanywe na mwana huyo?
7. Mtoto huyu angeitwajina gani na nini maana jina lake?
8. Ni habari njema ipi ambayo angewaambia Israeli?
9. Ni ishara gani ambayo malaika alimpatia Zakaria?
10. Ni jinsi gani Zakaria alivyowajulisha watu mtoto wake ataitwa jina gani?
11. Ni jambo gani la kushangaza lililotokea baada ya Zakaria kuandika jina la mwana wake ili watu waone ?
12. Yohana alipokua alikwenda kuishi wapi?

### Majibu ya Kina

13. Eleza kilichotokea katika nyumba ya Mungu wakati Zakaria alipokuwa akihudumu-ndani
14. Eleza habari ya kuzaliwa kwa Yohana Mbatizaji na jinsi alivyoitwa jina?
15. Ni kwa vipi Zakaria na Elisabeti ni mfano mzuri kwetu kufuata?

### Mjibu ya Nyongeza

16. Ni manabii gani waliotabiri kuja kwa Yohana Mbatizaji?